



STRATEGIC  
IMPACT  
ADVISORS

Biashara Yake, Maisha Yake



# Usimamizi wa Orodha ya Mali

—  
Usimamizi wa Biashara na Ujuzi  
wa Kusoma na Kuandika wa  
Kidijitali kwa Wanawake  
Wajasiriamali Wadogo

*Ripoti hii imeweza kufanikishwa kwa ushirikiano wa ukarimu na watu wa Marekani kupitia Uwakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID). Muongozo huu ulitolewa chini ya Mradi wa Frontia za Kidijitali za DAI (Cooperative Agreement AID-OAA-A-17-00033) kutokana na ombi la USAID wakishirikiana na Mastercard.*

# Taaswira ya Moduli



## Jedwali la yaliyomo

**Sehemu ya 1:** Usimamizi wa orodha ya mali ni nini? 7

**Sehemu ya 2:** Jinsi ya kusimamia orodha ya mali yako 15

**Sehemu ya 3:** Mifumo ya usimamizi ya orodha ya mali (kutumia mkono na kidijitali) 29



## Malengo


1. Kuelewa msingi wa usimamizi wa orodha ya mali.
2. Kujifunza kuhusu mifumo ya usimamizi wa orodha ya mali.

## Kwenye Moduli hii, unaweza...

- kutambua na kufanyia mazoezi mikakati ya kusimamia orodha ya mali yako
- kufanya mazoezi kwa kutumia mifumo ya mkono na kidijitali kwenye orodha ya mali

# Ni Changamoto Gani Unazopitia Dukani Kwako?

**Sasa Tuelezane  
tajriba zetu!**



**Huwezi kufuatilia  
bidhaa zako dukani.**



**Una bidhaa nyingi  
au chache  
dukani.**




**Hujui nini cha  
kutumana na wakati  
wa kutumana  
bidhaa.**



**Huwezi kujua bidhaa  
zinazouzika vyema  
na zisizouzika vyema.**



**Bidhaa zako  
huharibika mara kwa  
mara.**



**Huwezi kuamua bidhaa  
za kuacha kuuza na  
bidhaa za kuuza kwa  
diskaunti.**




**Unapoteza wateja  
kwasababu kuna foleni  
ndefu ya kuingia dukani  
kwako.**

 **Hebu  
wazia hili!**

Ratana anamiliki duka. Wakati wa kiangazi, huondoa baadhi ya bidhaa dukani ambazo hazihitajiki sana, kama vile miavuli. Hata hivyo, kuna siku mteja alimuulizia mwavuli, na hakupata mwavuli dukani. Baadaye, aligundua kuwa boksi la miavuli lililokuwa dukani limeanguka chini na kuharibu miavuli yote.

**Umelewa nini kutokana na hili tukio? Ni vipi Ratana angeepukana na hali hii?**





## RATANA



Alipoteza  
wateja



Alikosa  
mauzo



Alikosa  
pesa

Ratana angeepukana na hali hii kama  
angekuwa na mfumo wa usimamizi wa  
orodha ya mali.

# SEHEMU YA 1: USIMAMIZI WA ORODHA YA MALI NI NINI?

## Malengo:

1. Kujifunza kuhusu usimamizi wa orodha ya mali.
2. Kuelewa faida za usimamizi wa orodha ya mali.

Una ufahamu wa  
usimamizi wa  
orodha ya mali?



# Orodha Ya Mali Ni Nini?



Orodha ya mali ni bidhaa za vitu ambavyo biashara yako lazima iwe navyo dukani leo na siku za baadaye.

# Usimamizi wa Orodha ya mali

**Usimamizi wa orodha ya mali ni jinsi ambavyo unafuatilia na kudhibiti bidhaa za biashara yako wakati zinanunuliwa, hifadhiwa na kuuzwa.**

Mfumo wa usimamizi wa orodha ya mali husaidia kuhakikisha una idadi ya kutosha ya bidhaa kwa wakati na mahali zinapofaa kuwa.

**Kusimamia kuingia na kutoka kwa bidhaa kuanzia zinaponunuliwa hadi zinapouzwa.**





# Kwa maneno mengine ...

Usimamizi wa orodha ya mali hukusaidia ...



**Kufuatilia bidhaa  
zako.**



**Kujua wakati  
wa kuagiza.**



**Kujua nini cha  
kuagiza na  
kiasi gani.**



# Faida za Mfumo Unaofaa wa Usimamizi wa Orodha ya Mali


## 1. ENDESHA BIASHARA YAKO SAWA SAWA

Ikiwa duka lako haliwezi kusimamia orodha ya mali vizuri, basi biashara yako itapata shida.

*Kwa mfano, Ratana anahitaji kulinganisha bidhaa anazonunua na mahitaji ya wateja.*

Ikiwa atanunua zaidi ya zile atakazouza, atahitaji mahali pakuziweka zile zitakazobaki, na itabidi asubiri kurudisha gharama zake alizonunulia bidhaa, ambazo zinaweza kupunguza faida yake.

Ikiwa atapungukiwa na bidhaa zozote, atapoteza mapato ambayo yangepatikana ya bidhaa hiyo.



## 2. KEEP CUSTOMERS HAPPY



### Ni vipi wateja wako wanaweza kupata bidhaa kwa haraka?

- Lenga kuwa na bidhaa tayari dukani, hii inamaanisha unatakiwa kufuatilia wakati unaofaa kuagiza bidhaa.



### Wewe unapatikana vipi?

- Wateja wako wanatakiwa kuwa na uhakika kuwa watapata wanachotaka kikiwa dukani.
- Bidhaa zako zote zinatakiwa kuwa za hivi karibuni na hazijaharibika. Bidhaa ambazo zimeharibika kidogo, na bidhaa ambazo muda wake wa kukaa umekaribia kuisha zinafaa ziuzwe kwa diskaunti.



### Ni kwa uharaka gani unaweza kuelewa mahitaji ya wateja wako?


- Agiza bidhaa au chapa mpya ikiwa kuna wateja wanahitaji.

**Kuna uwezekano mkubwa wateja kurudi tena kununua bidhaa kwako ikiwa wanajua wazi kuwa duka lako lina bidhaa wanazohitaji.**

### 3. SIMAMIA KUKUA KWA BIASHARA YAKO



Wakati biashara yako inakua, vile vile usimamizi wako wa orodha ya mali unahitajika kuwa na mpango mzuri.



Ni muhimu kuwa na udhibiti wa bidhaa zako halisi kuanzia siku ya kwanza ikiwa unapanga kupanda daraja. Kwa kuweka mfumo wa orodha ya mali unaofaa mapema ni muhimu kwa usimamizi wa bidhaa zako dukani.



## 4. TATHMINI UTENDAJI KAZI WA BIASHARA YAKO

**Weka viashiria ambavyo unaweza kutathmini kila mwezi ili uweze kufuatilia mwelekeo wa biashara yako. Sasa tupitie baadhi ya sampuli za viashiria:**

- Ni hasara kiasi gani ulipata kutokana na bidhaa ambazo hazikununuliwa? Jaribu kuangalia ikiwa kuna bidhaa zinazosababisha hizi hasara.
- Ni hasara kiasi gani ulipata kutokana na bidhaa ambazo muda wake wa kukaa ulikuwa umeisha? Jaribu kuboresha mfumo uliopo wa kuuza vitu vinavyoharibika haraka kwa diskaunti.
- Kuna bidhaa ambazo kawaida hazipatikani dukani? Hakikisha kuongeza idadi ya vitu ukiagiza.

**Unaweza kutathmini utaratibu wa orodha ya mali yako:**

- Ni wasambazaji gani wa kutegemewa, na ni wapi wasioweza kutegemewa? Ikiwa kuna wasambazaji bidhaa ambao hawatimizi oda zao kwa wakati, huu ndio wakati wa kutafuta wengine wapya.
- Ikiwa umetengeneza uhusiano mzuri wa kibiashara na wasambazaji wako, unaweza kuomba diskaunti.
- Una wasambazaji ambao wanauza bei ya juu kuliko washindani wao? Waambie wakuuzie bei nzuri au ubadilishe wasambazaji.



## SEHEMU YA 2: JINSI YA KUSIMAMIA ORODHA YA MALI YAKO

**Malengo:** Kuwa na ufahamu wa vidokezo na ujanja wa kusimamia orodha ya mali yako.

Sasa tujifunze  
jinsi ya  
kusimamia  
orodha ya mali  
yako!



Sasa kwasababu  
umejua mfumo  
wa usimamizi wa  
orodha ya mali ni  
nini...

Nani  
anayesimamia  
usimamizi wa  
orodha ya mali  
ya biashara  
yako?

Unaweza kuorodhesha  
baadhi ya faida za  
wanaume na wanawake  
wanaosimamia usimamizi  
wa orodha ya mali?



# Nani Anafaa Kusimamia Orodha ya Mali?

**Usimamizi wa orodha ya mali ni ujuzi wa kujifunza na inamchango mdogo sana kuhusiana na jinsia uliyonayo. Mtu yeyote akipewa nafasi ya kujifunza ujuzi huu na kufanya mazoezi, awe mwanamume au mwanamke, anaweza kufaulu!**

Wanaume na wanawake wanaweza kuwa na tajriba zaidi ya kutumia bidhaa tofauti unazouza dukani kwako. Kwa mfano, wanawake wanaweza kutumia bidhaa tofauti za nyumbani kuliko wanaume kwenye maisha yao ya kila siku, hii ikimaanisha kuwa wana elimu kuhusu aina za bidhaa za nyumbani wanazoweza kuuza kwenye maduka yao.

Mwanamke anaweza kupendekeza bidhaa kulingana na tajriba yake, na pia anaweza kuwasihi wanawake wenzake, hivyo basi kuongeza mauzo na faida kwa biashara.

Kuwa na wanawake wanaoweza kusimamia mchakato wa usimamizi wa orodha ya mali inaleta maana kubwa kwenye biashara!







Sofia, nahitaji kuondoka nina miadi na watu wa benki. Yule msambazaji mpya wa maziwa amechelewa. unaweza kuzungumza naye kuhusu bei zake ikiwa atakuja wakati nimeondoka?

Huko ni kukosa heshima! Mbona hukuniambia?

Sikugundua mambo haya kabla! Tutakutana na msambazaji pamoja na wewe, lakini nadhani ni muhimu kukomesha watu wenye fikra kama hizo.

Na nitakwepo kukusaidia wakati wa mazungumzo!



Hmm... wakati ule nikiwa peke yangu nikishauriana na msambazaji mpya, alikuwa ananisukuma sana kuhusu kutupatia bei za juu, lakini ulipoingia dukani, tabia yake ilibadilika, na akateremsha bei.

Sikufikiria sana kuhusu hilo jambo. Lakini nakumbuka, nina hakika alinitendea tofauti kwasababu mimi ni mwanamke. Labda unaweza kuvunja miadi na benki ili uzungumze na msambazaji?

Sawa, nitaendelea kuwa na muingiliano na washirika wa kiume wenye biashara. Hapo ni kweli: nikiona anajaribu kujinufaisha kutokana na hali iliyopo, nitamuaibisha kwa hiyo tabia yake!

Ushawahi kutokewa na hali kama ya Sofía?  
Kama ishawahi kukutokea, ulifanyaje?  
Labda ungekuwa umefanya jambo tofauti?



# Ni vipi unaweza kusimamia orodha ya mali yako?

## 1. PANGA BIDHAA NA MAELEZO YA MSAMBAZAJI

- Orodhesha maelezo yote ya bidhaa maalum, kama jina la bidhaa, idadi, chapa, bei ya kununulia, bei ya kuuzia, tarehe ya kuharibika, na mahali bidhaa zilipo.
- Rekodi maelezo ya msambazaji, kama vile jina la msambazaji, maelezo ya mawasiliano, gharama ya jumla, na kiwango cha kima cha chini cha kuagiza.



## 2. WEKA BIDHAA DUKANI

Ni tofauti gani  
iliyopo kati ya  
rafu za maduka  
haya mawili?



- ❑ Onyesha bidhaa zote katika mpangilio mzuri. Bidhaa ambazo hazitawekwa vizuri na kuonekana inamaanisha kutakosekana mauzo na kupoteza mapato.
- ❑ Fuata utaratibu wa bidhaa wa kwanza-kuingia, kwanza-kutoka. weka bidhaa zilizotangulia kunuliwa mbele kwenye rafu ili kuhakikisha zinauzwa kwanza, kabla muda wake wa kukaa haujaisha.
- ❑ Tambua ni bidhaa gani zinazonunuliwa haraka, zile ambazo zina mauzo ya wastani, na zile ambazo zina mauzo ya chini.
- ❑ Weka bidhaa za kutosha dukani zile zinazonunuliwa haraka. Zingatia kutoa diskaunti kwa bidhaa ambazo hazinunuliwi vizuri.



### 3. FANYA HESABU YA BIDHAA KILA BAADA YA MUDA

- Kuhesabu bidhaa zako kila baada ya muda kutakuhakikishia kuwa na rekodi sahihi na za wakati, ili kuepusha uharibifu, dosari na vitu kurudisha.
- Kuhesabu kutakusaidia kuelewa ni bidhaa gani zinazonunuliwa haraka na zipi ambazo hazinunuliwi haraka, na kutokana na maelezo hayo, unaweza kupanga wakati na kiasi cha kuagiza kila bidhaa.
- Kuhesabu kunaweza kufanyika kila baada ya muda, kama vile kila baada ya wiki moja au mbili. Lakini kumbuka, kuhesabu bidhaa zenyewe kunaweza kuchukua muda mwingi na gharama.
- Mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa orodha ya mali unafanya mchakato wa kuhesabu kuwa mwepesi na rahisi. Ikiwa una mauzo mengi au unapanga kupanua biashara yako, unaweza kuzingatia kubadilisha na kutumia mfumo wa kidijitali.



#### 4. KUTENGENEZA MCHAKATO WA UNUNUAJI



- Kulingana na salio la bidhaa zako dukani kwa sasa, orodhesha bidhaa ambazo zimeuzwa au zimepungua na zinahitaji kuagizwa tena.
- Kwa kutumia orodha hii, weka oda ya ununuzi kwa wasambazaji wako wa bidhaa.
- Ikiwa utatumia mfumo wa kidijitali, unaweza kuweka ilani na tahadhari bidhaa zinapopungua, ili ujue ni wakati wa kuagiza.



## 5. TENGENEZA MCHAKATO WA KUPOKEA BIDHAA



- Ni muhimu kukagua vitu vyote vilivyopokelewa dhidi ya oda ya ununuzi ili kupunguza hasara kutokana na makosa ya msambazaji, ya kuleta bidhaa ambazo muda wake wa kukaa umeisha, bidhaa zilizoharibika, au bidhaa zilizopotea njiani.
- Ukipokea bidhaa zako, unatakiwa kuhesabu na kufungua mizigo yote na kukagua orodha ya mzigo, ankara, na vitu ulivyopokea dhidi ya oda ya ununuzi halisi.






## 6. ANZISHA MCHAKATO WA DISKAUNTI NA UTANGAZAJI WA BIDHAA



- Ikiwa mauzo ya bidhaa yamepungua kutokana na mambo ya misimu au mielekeo, unaweza kutoa punguzo la bei na diskaunti ili kuleta mauzo. Kwa mfano, Ratana aliweka miavuli dukani wakati wa kiangazi. Angekuwa ametoa diskaunti ili kuchochea ununuzi.



- Kwa utangazaji wa bidhaa, unahitaji kuhakikisha kuwa una bidhaa za kutosha dukani ili kukidhi mahitaji ya wateja.



## 7. TAFUTA UTARATIBU WA BIDHAA ZILIZORUDISHWA



- Mteja akirudisha kitu ambacho kimeharibika au kinadosari, kinafaa kutengenezwa au kurudishwa kwa msambazaji.
- Ikiwa kitu kinatengenezeka lakini mteja hakitaki tena, kijumlishe kwenye hesabu ya orodha ya mali yako na ukiweke mahali panapofaa kukiuzua.
- Unaweza pia kutenga nafasi kwenye duka lako kuweka bidhaa ambazo zimeharibika au kurudishwa.



# Mambo Makuu ya Kuzingatiwa



- 1. Wanaume kwa wanawake wanaweza kushughulikia usimamizi wa orodha ya mali.** Kwa kufanya mazoezi, mtu yeyote anaweza kushughulikia usimamizi wa orodha ya mali! Pia wanawake wanaweza kutumia elimu yao kutoa mapendekezo kwa baadhi ya bidhaa kwa wateja wa kike.
- 2. Uwe na mpangilio wa maelezo na bidhaa zako.** Inaweza kuwa vigumu kufuatilia maelezo muhimu ya bidhaa zote ulizonazo dukani. Chukua muda zaidi kurekodi maelezo muhimu kuhusu orodha ya mali yako, na uhakikishe unapanga vizuri bidhaa zako ili kufanya duka lako livutie.
- 3. Iwe kawaida kufanya usimamizi wa orodha ya mali.** Kufuatilia na kusimamia bidhaa zako lazima kufanyike mara kwa mara ili kuhakikisha una maelezo halisi kulingana na wakati. Jaribu kuwa na mazoea ya kupokea bidhaa zako mara kwa mara na kuzihesabu ili usimamizi wa orodha ya mali uwe ni kawaida yako.
- 4. Kuwa mbunifu.** Ikiwa unaona baadhi ya bidhaa hazinunuliwi vizuri, fikiria mbinu tofauti za kuwachochoea wateja kununua hizo bidhaa. Kwa mfano, ni aina gani ya diskaunti unaweza kutoa? Ni vipi unaweza kupanga hizi bidhaa ili kuhimiza wateja kununua?

## SEHEMU YA 3: MIFUMO YA USIMAMIZI YA ORODHA YA MALI (KUTUMIA MKONO NA KIDIJITALI)

**Malengo:** Kuelewa mbinu za kusimamia orodha ya mali yako kwa kutumia mkono na kidijitali.


Unatumia mkono au kidijitali kwenye usimamizi wa orodha ya mali?



Kufuatilia bidhaa zako kunaweza kuchosha. Lazima ubadilishe utumie mfumo unaofaa wa kushughulikia orodha ya mali yako.



## MIFUMO YA USIMAMIZI YA ORODHA YA MALI



# Tumia Mkono

## A. SAJILI YA UNUNUZI

Sajili ya ununuzi inaweza kukusaidia kuweka akaunti ya kina ya vitu ambavyo vilinunuliwa kutoka kwa msambazaji, siku viliponunuliwa, kiasi chake, na kwa bei gani.

Unaweza pia kurekebisha sajili kulingana na hali ya sasa ili kuorodhesha:

- Maelezo ya bidhaa – kama vile jina la bidhaa, idadi, chapa, bei ya kununulia, bei ya kuuzia, tarehe ya mwisho ya muda wa kukaa, na mahali bidhaa zilipo.
- Maelezo ya msambazaji – kama vile jina, nambari za mawasiliano, gharama ya jumla, na kiwango cha kima cha chini cha kuagiza.



## A. SAJILI YA UNUNUZI

Tarehe	Jina la Msambazaji	Vitu vilivyonunuliwa	Kiasi kilichonunuliwa (A)	Bei ya kitu kilivyonunuliwa (B)	Kiwango cha jumla (A*B)	Bei ya kitu kilivyouzwa
01/07/2022	ABC Msambazaji	Sabuni	100	20	2,000	23



# Tumia Mkono



## B. SAJILI YA BIDHAA

**Kuhesabu bidhaa kunaweza kufanyika kila baada ya muda, kama vile baada ya wiki moja au mbili, kwa kutumia sajili ya bidhaa.**

Kulingana na salio la bidhaa, unaweza kuelewa ni bidhaa gani zinanunuliwa haraka, zipi hazununuliwi haraka, na unaweza kupanga ni wakati gani na kiasi gani cha kuagiza kila bidhaa. Sajili pia inaweza kurekebisha ili kulingana na hali ya sasa na kuakisi kiwango cha bidhaa zilizoharibika, zenye dosari na zilizorudishwa.





## B. SAJILI YA BIDHAA

Tarehe	Kitu (vi)	Idadi ya vitu vinavyopatikana dukani: Kiasi (A)	Idadi ya vitu vilivyouzwa: Kiasi (B)	Salio la bidhaa (A-B)
01/07/2022	Pepsi	100	25	75





**Nahofia kuwa ikiwa nitasimamia orodha ya mali kwa mkono, nitapoteza maelezo yote ninayohitaji! Imani, Unajua kama kuna njia mbadala inayoweza kunisaidia?**

**Naam, bila shaka! Napendekeza ujaribu mifumo ya kidijitali ya orodha ya mali. Haiweki tu maelezo lakini pia zinakujulisha wakati unahitajika kuagiza vitu tena.**

**Hiyo inaonekana inafaa sana! Unajua baadhi ya mifumo hii? Na ni kifaa gani kinahitajika?**

**Kwa watu wengi, simu ya kisasa inatosha! Wacha nikuonyeshe baadhi ya mifano ya mifumo ya kidijitali ya orodha ya mali.**



# Mifumo ya Kidijitali ya Orodha ya mali

- Mifumo ya kidijitali ya Orodha ya mali ya kielektroniki hufuatilia bidhaa, vifaa, na bidhaa za biashara kupitia programu ya kompyuta kwa wakati. Mifumo hii inaweza kukusaidia kufanya maamuzi na utabiri wa ugawaji wa orodha ya mali au uagizaji bidhaa.
- Mifumo yote ya kutumia mkono na kidijitali inaweza kukusaidia kuwa na mipango, lakini mifumo ya kidijitali ya orodha ya mali huwa ni madhubuti sana. Mifumo ya kutumia mkono ya orodha ya mali, mambo mengine husahaulika akilini, kama kujua wakati wa kuagiza baadhi ya bidhaa. Mifumo ya kidijitali ya orodha ya mali hukuweka katika hali halisi ya kinachoendelea kwa kukujulisha mara kwa mara.
- Mifumo ya mkono ya orodha ya mali inaweza kupotea au kuharibika, programu za kidijitali huhifadhi maelezo yako. Ikiwa utakariri maelezo ya kuingia kwa akaunti yako, utaweza kufikia mfumo wako kutoka kwa kompyuta yoyote au simu ya kisasa.
- Baadhi ya mifumo ya kidijitali ya orodha ya mali huwa haipatikani bure, unaweza kupata mrejesho wa uwekezaji, kwasababu inaweza kusaidia kuongeza mauzo kwa ufanisi wao.



# Tumia Kidijitali



Sasa tufanye!

## MIFUMO YA KIDIJITALI YA USIMAMIZI WA ORODHA YA MALI

	<u>Odoo</u>	<u>ShipBob</u>	<u>Sortly</u>	<u>Tally</u>	<u>Zoho</u>
TEKNOLOJIA INAYOHITAJIKA	Simu ya kisasa / Kompyuta	Simu ya kisasa / Kompyuta	Simu ya kisasa / Kompyuta	Kompyuta	Simu ya kisasa / Kompyuta
GHARAMA	Bure	Kuanzia Dolla 5.38 kwa mwezi	Bei za kimatabaka zinapatikana	Dolla 360 kwa mwaka	Bure (masharti kutumika)
VIPENGELE VINGINE	Vyote vimedhibitiwa kwa nywila.				

# Tilia Mkazo: Jinsi ya kutumia Zoho

Sasa tuangalie yaliyojumuishwa kwenye mfumo wa kidijitali wa orodha ya mali ya Zoho.



ONGEZA VITU




SIMAMIA  
WASAMBAZAJI



ODA YA UNUNUZI




ORODHA YA BEI



USIMABJI UPAU



RIPOTI




MAFUNZO KAMILI

# Sasa Eleza kwa Muhtasari!



Sasa  
tuorodheshe  
uliyojifunza.

- Usimamizi wa orodha ya mali ni nini?
- Jinsi ya kusimamia orodha ya mali yako
- Mifumo ya usimamizi wa orodha ya mali
  - Mifumo ya kutumia mono (vitabu na sajili)
  - Mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa orodha ya mali




Tuma mashaka yako na  
maswali!

Ni kipi ulichoona kinafaa?  
Umejifunza nini leo?

Ni mfumo gani wa usimamizi  
wa orodha ya mali  
utakaotumia?





**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI

STRATEGIC  
**IMPACT**  
ADVISORS



[www.siaedge.com](http://www.siaedge.com)

Laini ya Pili  
Laini ya Tatu

